



# Ufunguo wa maisha

## Maoni ya wananchi juu ya umuhimu wa shule



### 1. Utangulizi

Nchini Tanzania, shilingi 25 kati ya 100 zinatengwa na serikali kwa ajili ya elimu. Licha ya hilo, mtoto mmoja kati ya watatu humaliza elimu ya msingi bila kujua kusoma na kuhesabu.

Sera mpya ya elimu imezinduliwa mwaka huu wa 2015. Elimu ya msingi sasa imepangiliwa kuwa ya miaka kumi badala ya miaka saba. Elimu hii itakuwa ni ya lazima kwa wote na wazazi hawatohitajika kulipa ada. Serikali imeahidi kufuta ada hii kuanzia mwaka 2016.

Hata hivyo, kwa upande wa elimu ya sekondari, ubora wake pia hauridhishi – hii inadhihirishwa na kuendelea kushuka kwa kiwango cha ufaulu katika mitihani ya Taifa. Sera hii mpya ni sehemu ya mkakati wa kujibu malalamiko ya wananchi kulikotokana na matokeo mabaya ya kidato cha 4. Hatua za kuinua ubora wa elimu ya sekondari ni pamoja na kuinua ari ya walimu na kuboresha miundombinu ya elimu.

Je, sera mpya itainua ubora wa kujifunza? Ni kwa kiasi gani inajibu matarajio na matamano ya mwananchi wa kawaida kwa watoto wake?

Katika muhtasari huu, tunatoa taarifa juu ya mawazo ya wananchi juu ya elimu, na hasa ubora wa elimu ya sekondari. Madodoso yaliyotumika kupata taarifa hii yaliandaliwa kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WEMU). Takwimu zilikusanywa kati ya tarehe 5 na 22 Novemba 2014 katika sampuli yenye uwakilishi wa kitaifa. Utafiti huu wa *Sauti za Wananchi* ulifanywa kwa njia ya simu za mkononi. Takwimu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,381, na ni wakilishi kwa Tanzania Bara. Kwa taarifa kuhusu duru zilizopita (pamoja na data, madodoso, na taarifa), tembelea [www.twaweza.org/sauti](http://www.twaweza.org/sauti).

Muhtasari huu umeandikwa na Angela Ambroz and Elvis Mushi  
Na umeandaliwa na Twaweza East Africa.  
Umetolewa Julai 2015

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.  
Simu: +255 22 266 4301 | [uwazi@twaweza.org](mailto:uwazi@twaweza.org) | [www.twaweza.org/sauti](http://www.twaweza.org/sauti)



Matokeo muhimu kwenye muhtasari huu ni:


- Mwananchi mmoja kati ya wawili anaamini kwamba kujua kusoma na kuandika ni stadi muhimu kwa wanaomaliza elimu ya sekondari.
- Wananchi sita kati ya kumi wanaamini kwamba elimu ya msingi inawaandaa wanafunzi vizuri kuendelea na elimu ya sekondari.
- Karibu wananchi wawili kati ya watatu wanaamini kuwa watoto wanapaswa kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza katika shule za msingi na sekondari.

## 2. Mambo sita katika maoni ya wananchi kuhusu sekta ya elimu Tanzania

### Jambo la 1: Kuna tofauti za rika katika fursa za elimu

Wananchi wengi (67%) wamepata elimu ya msingi (Kielelezo cha 1). Wengine 11% wamemaliza elimu ya sekondari (Kielelezo cha 1).

**Kielelezo cha 1: Stadi za elimu za Watanzania**



**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* Utafiti kwa simu za mkononi – Duru ya Awali (2012)


Walipoulizwa juu ya watoto wao, idadi kubwa (65%) waliripoti kuwa na watoto (wavulana au wasichana) waliomaliza elimu ya msingi. Pamoja na hayo, asilimia 26 waliripoti kuwa na mtoto anayesoma shule ya sekondari; ni asilimia 8 waliokuwa na watoto katika chuo kikuu au elimu ya baada ya sekondari (takwimu hazikuonyeshwa).

Hivyo basi, wakati asilimia 11 wameripoti kumaliza elimu ya sekondari, asilimia 26 wameripoti kuwa wana mtoto wa kiume au wa kike katika shule ya sekondari – jambo linaloonyesha kuongezeka kwa fursa za elimu ya sekondari kwa rika la vijana wa Tanzania. Sera mpya ya 2014 imeweka mwaka mmoja wa elimu ya awali ya lazima, bila malipo ya ada. Hakuna mashaka kuwa lengo la Tanzania la kuongeza fursa za elimu, kwa ngazi mbalimbali, lina matokeo chanya katika uandikishaji. Watoto wengi zaidi kuliko hapo nyuma wanaenda shule.

## Jambo la 2: Matarajio kwa wahitimu wa elimu ya sekondari ni madogo

Tuliwauliza wananchi wanategemea wanafunzi wanapomaliza kidato cha 4 wajue nini, na jibu lililotolewa na wengi (asilimia 49) ni kujua kusoma na kuandika (Kielelezo cha 2). Haya ni matarajio ya chini sana kwa mtu aliyetumia miaka kumi shuleni. Jibu la pili kutoka kwa wengi ni kwamba wanaohitimu kidato cha 4 wawe na stadi za kiufundi zinazoweza kuwafanya wajajiri (Kielelezo cha 2). Matarajio haya yamo katika sera mpya ya 2014 inayohakikisha kwamba kujua kusoma na kuhesabu na stadi za uchambuzi na ubunifu zinakuzwa shuleni (sehemu 3.2.4 hadi 3.2.6 za sera).

### Kielelezo cha 2: Je, stadi muhimu kwa anayehitimu kidato cha 4 ni zipi?




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* Utafiti kwa simu za mkononi – Duru ya 27 (Novemba 2014)

## Jambo la 3: Wazazi wanatarajia watoto wao wawe madaktari au waalimu

Tuliwauliza wazazi wanatarajia watoto wao wafanye kazi gani. Jibu la wengi lilikuwa “daktari” au “mwalimu” (Kielelezo cha 3 - asilimia 29 na 27). Majibu haya kwa namna moja au nyingine yanapingana na matarajio waliyonayo wazazi juu ya kitu gani watoto wao watajifunza katika shule ya sekondari.

### Kielelezo cha 3: Je, wazazi wanataka watoto wao wapate kazi zipi?




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* Utafiti kwa simu za mkononi – Duru ya 27 (Novemba 2014).  
Data katika chati hii inatokana na wazazi wenye watoto sekondari tu.  
Kwa data kamili angalia: [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org).

### Jambo la 4: Wananchi sita kati ya kumi wanaamini kuwa elimu ya msingi inawaandaa wanafunzi vizuri kuendelea na elimu ya sekondari

Wananchi wengi wana imani na mfumo wa elimu; kwamba elimu ya msingi inawaandaa wanafunzi vizuri kuendelea na elimu ya sekondari. Wananchi sita kati ya kumi (asilimia 64) wanaamini hivyo (figure 4). Cha kushangaza ni kwamba, wahitimu wengi wa kidato cha 4 waliopitia shule za umma za msingi na sekondari hawaamini hivyo. Nusu yao tu ndio wanaoamini kwamba shule za msingi zinawaandaa wanafunzi vizuri kuendelea na elimu ya sekondari (figure 4).

### Kielelezo cha 4: Je, stadi zinazopatikana katika shule za msingi zinawapa wanafunzi misingi imara kwa ajili ya elimu ya sekondari?




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* Utafiti kwa simu za mkononi – Duru ya 27 (Novemba 2014).

## Jambo la 5: Wananchi wengi wanataka watoto wao wafundishwe kwa lugha ya Kiingereza katika shule za msingi na sekondari

Wakati wananchi wengi kiasi wanaamini kwamba elimu ya msingi inawaandaa watoto vizuri kuendelea na elimu ya sekondari, karibu wazazi wote wenye watoto sekondari wanakubali kwamba mabadiliko ya lugha husababisha matatizo. Asilimi 89 ya wazazi wenye watoto sekondari wanakubali kwamba kubadili ya lugha kutoka Kiswahili (shule za msingi) kwenda Kiingereza (shule za sekondari) kunaleta matatizo (Kielelezo cha 5).

### Kielelezo cha 5: Je, wanafunzi wanatatizwa wakati wa kubadili lugha ya kufundishia kutoka shule ya msingi kwenda ya sekondari?



**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* Utafiti kwa simu za mkononi – duru ya 27 (Novemba 2014).  
Data katika chati hii inatokana na wazazi wenye watoto sekondari tu.  
Kwa data kamili angalia: [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org).

Tuliwauliza juu ya matatizo halisi yanayosababishwa na mabadiliko ya lugha, majibu ya wengi yalikuwa:

- “Inachukua muda kujirekebisha.” (52%)
- “Inaathiri uwezo wao wa kujifunza.” (31%)

Ufumbuzi wa tatizo hili kwa wengi ulikuwa: **“Kiingereza kiwe lugha ya kufundishia katika shule za msingi na sekondari.” (63%)**. Hata hivyo, sera mpya inapenda Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia katika shule za msingi na sekondari.

## 3. Hitimisho

Jamii iliyoelimika ni msingi wa maendeleo ya taifa. Elimu imeonekana kuwa na uhusiano chanya na afya bora, kipato cha juu, na kupungua kwa kasi ya kuzaana. Kuwekeza katika elimu bora kunapaswa kuwa kipaumbele cha serikali yoyote.

Hapa Tanzania sekta ya elimu imekuwa nyumba kiufanisi. Hivi karibuni, tathmini ya Uwezo yenye data za 2013, imeonyesha kwamba ni asilimia 56 ya watoto wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 10 na 16 wenye uwezo wa kufaulu mtihani wa kusoma. Kuna haja ya kuinua ubora wa kujifunza kwa haraka lakini swali la msingi ni: kwa njia gani?

Mwezi Februari 2015, Rais Jakaya Kikwete alizindua sera mpaya ya Elimu na Mafunzo. Sera hii inahusisha, pamoja na mambo mengine, kubadili sera ya lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu ambapo sasa lugha zote mbili za Kiswahili na Kiingereza zinatambuliwa kuwa lugha za kufundishia na Kiswahili kimepewa uzito zaidi ya Kiingereza. Hatua hii kwa kiasi fulani inajibu malalamiko ya muda mrefu kuhusu lugha sahihi ya kufundishia ambapo wadau wengi wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, stadi za Kiingereza zinahitajika sana hata katika soko la ajira hapa Tanzania. Kujitoa katika kufundisha na kujifunza Kiingereza, (hasa kwa kuwa uwezo wa sasa katika Kiingereza ni wa chini), kutawaathiri vibaya vijana wanataka kujiunga na soko la ajira linaloongezeka hivi sasa. Kuhusu swala hili, wazazi wanatoa kauli – asilimia 63 wanapenda lugha ya kufundishia iwe Kiingereza katika shule za msingi na sekondari (Jambo la 5).

Pengine jambo la ‘kutisha’ lililowekwa wazi na toleo hili la *Sauti za Wananchi*, linahusu matarajio ya wazazi. Nusu yao wanaamini kuwa anayehitimu elimu ya sekondari lazima ajue kusoma na kuandika kwa ufanisi. Hii ina maana kuwa matarajio ya wazazi ni kwamba watoto wao watamaliza shule wakiwa na stadi ambazo walistahili kuwa nazo katika miaka ya mwanzo ya elimu ya msingi. Toleo la Julai 2014 la *Sauti za Wananchi* lilikuwa na matokeo yanayofanana na haya: asilimia 31 tu ya wazazi walifikiri kuwa watoto wanaomaliza darasa la 2 wangepewa kumudu stadi za darasa la 2. Lakini asilimia 10 kati yao waliamini kwamba walikuwa wamejifunza stadi hizo.<sup>1</sup> Matarajio madogo kiasi hiki ya mfumo wa elimu yanazaa duara la balaa, ambapo matokeo ni ya chini lakini wazazi wanayaona kuwa ni sawa. Hili jambo limewafanya watunga sera, walimu na viongozi wa elimu kutokuwa na nia ya kuchukua hatua rekebisho.

Ni mapema mno kutathmini sera hii mpya ya Elimu na Mafunzo. Lakini inatia moyo kwamba, inatoa nafasi kubwa kwa wadau kushiriki katika utekelezaji wake. Ni muhimu kwa wazazi, wanafunzi na wataalamu wa elimu pamoja na asasi za kiraia kuchukua nafasi hii kwa shauku kubwa. Umiliki wa aina hii utasaidia kukuza matarajio ya jamii juu ya elimu ya msingi na sekondari. Hii inaweka nguvu mpya katika utekelezaji wa sera pamoja na kuipa uwezo wa kuigeza elimu ya Tanzania kuwa yenye uwezo wa kuhakikisha kuwa watoto wanajifunza na kukuza stadi zinazohitajika katika dunia ya karne ya 21.

---

<sup>1</sup> *Sauti za Wananchi*, What’s going on in our schools, Brief No. 13, July 2014



